**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# MPANGO WA KITAIFA WA HIFADHI YA MAZINGIRA YA BONDE LA MTO RUAHA MKUU



**Mei, 2017**

**ORODHA YA VIFUPISHO**

| | |
|---|---|
| EIA | Environmental Impact Assessment |
| IWRMDP | Integrated Water Resources Management and Development Plan |
| JFM | Joint Forest Management |
| KUU | Kamati ya Ulinzi na Usalama |
| RBWB | Rufuji Basin Water Board |
| RUBADA | Rufiji Basin Development Authority |
| SAGCOT | Southern Agriculture Growth Corridor of Tanzania |
| SEA | Strategic Environmental Assessment |
| TAMISEMI | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TANAPA | Tanzania National Parks |
| TANESCO | Tanzania Electric Supply Company Limited |

**DIBAJI**

Bonde la Mto Ruaha Mkuu ni moja kati ya mabonde manne yanayounda Bonde la Rufiji ambapo mabonde mengine ni Kilombero, Luwegu na Rufiji Chini. Eneo la Bonde la Mto Ruaha Mkuu lina ukubwa wa kilometa za **mraba 85,554** ambazo ni sawa na **asilimia 47** ya eneo lote la Bonde la Rufiji. Bonde hili linajumuisha Mikoa Saba ambayo ni Iringa, Njombe, Mbeya, Morogoro, Dodoma, Singida na Tabora. Bonde la Mto Ruaha Mkuu linaundwa na mito mikubwa ya Mbarali, Ruaha, Kimani, Kisigo, Lukosi, Ruaha Mdogo, Ndembela na Chimala.
Bonde la Mto Ruaha Mkuu ni maarufu kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi kama kilimo, ufugaji, uvuvi, uchimbaji mdogo wa madini, viwanda vidogo, uhifadhi na utalii. Vilevile, Bonde la Mto Ruaha Mkuu hutumika kwa kilimo cha umwagiliaji, ambapo zaidi ya wakulima 45,626 hutumia maji hayo kwa umwagiliaji katika eneo la hekta hekta 77,187 kati ya hekta 126,816 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Aidha, maji hayo hutumika kwa uzalishaji wa umeme katika mabwawa ya Mtera na Kidatu ambapo Kidatu pekee huzalisha megawati 204 wakati Mtera huzalisha megawati 80. Kwa upande wa shughuli za uhifadhi wa mazingira, maji ya bonde hili hutumika kama chanzo kikuu katika ustawi wa ikiolojia ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Kwa upande wa shughuli za kijamii, maji ya Mto Ruaha Mkuu hutumika kukidhi mahitaji ya majumbani kwa wakazi wanaoishi katika bonde hilo.

Pamoja na umuhimu huu, kuanzia miaka ya 1990, Bonde la Mto Ruaha Mkuu limekuwa likikabiliwa na changamoto mbalimbali za uharibifu wa mazingira na hivyo kuathiri mfumo-ikolojia yake. Kutokana na changamoto hiyo, serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikichukua hatua zinazoendana na utekelezaji wa Sera na Sheria mbalimbali ili kuokoa ikolojia ya Bonde hili.

Kwa kutambua ukubwa wa tatizo na hasara itokanayo na uharibifu wa mazingira katika bonde hili, Ofisi ya Makamu wa Rais iliunda kikosi kazi cha kitaifa cha kufanya tathmini ya visababishi na kutoa mapendekezo kuhusu hatua zinazofaa kuchukuliwa ili kuongoa mazingira na huduma za bonde hilo kiikolojia, kijamii na kiuchumi.

Mpango huu ni matokeo ya kazi ya Kikosi Kazi cha Kitaifa ambacho kilitembelea eneo lote la Bonde la Mto Ruaha Mkuu ikiwemo baadhi ya maeneo ya vyanzo vya maji yaliyopo katika wilaya za Makete, Wanging'ombe, Mbeya, Mufindi, Iringa, Kilolo na Chunya; maeneo yenye matumizi makubwa ya maji yanayozunguka Eneo Oevu la Ihefu; na maeneo yanayopokea maji kutoka kwenye Eneo Oevu la Ihefu wilayani Mbarali ikiwemo Bwawa la Mtera na hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Mpango kazi huu unaonyesha visababishi vya uharibifu wa mazingira, mapendekezo ya hatua za kuchukua ili kuokoa bonde la Mto Ruaha Mkuu, ambayo yameainishwa katika ngazi ya Kisera, Kisheria, Kimkakati na Kiutendaji.

Ofisi ya Makamu wa Rais inatoa pongezi na shukurani nyingi kwa kazi nzuri iliyofanywa na Kikosi Kazi na tunatarajia utekelezaji wenye tija. Aidha, Serikali inategemea ufanisi mkubwa katika kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa.

---------------------------------------------------------------------

**Mhe. January Y. Makamba (Mb.)**
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MUUNGANO NA MAZINGIRA**

**TAMKO LA MHE. MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KUHUSU RASIMU YA MPANGO WA KUHIFADHI IKOLOJIA YA MTO RUAHA MKUU**

Bonde la Mto Ruaha Mkuu ni muhimu sana kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa maendeleo ya taifa letu. Miongoni mwa utajiri wa asili kwenye bonde hili ni pamoja na ardhi oevu ya Usangu yenye ustawi wa bioanuai na uhakika wa upatikanaji wa maji kwa jamii katika ukanda wa chini hasa mabwawa ya Mtera na Kidatu ambako umeme hufuliwa kwa maporomoko ya maji. Vilevile, bonde hili ni muhimu kwa shughuli za kilimo na ufugaji, uvuvi, utalii, usafirishaji na uchakataji wa mazao ya chakula.

Pamoja na umuhimu huo, bonde hili linakabiliwa na uharibifu mkubwa wa mazingira, hususan, uharibifu wa mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji. Uharibifu huu unatokana na shughuli za kibinadamu zisizo endelevu unaofanywa katika maeneo ya vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na kwenye vilele vya milima, kwenye miteremko ya milima na katika mabonde.

Ofisi yangu na wadau mbalimbali wamekuwa wakifanya jitiahada za kutunza mazingira ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi endelevu ya rasilimali zilizopo kwenye bonde. Jitihada hizo ni pamoja na uundwaji na utekelezaji wa sera na sheria mbalimbali zinazohusiana na shughuli za kiuchumi na kijamii zinazofanyika katika bonde. Aidha, kumekuwa na utekelezaji wa mipango, programu, mikakati na miradi mbalimbali kwa lengo la kuhifadhi mazingira na ikolojia ya Bonde la mto huo. Pamoja na jitihada hizo, hali ya ikolojia ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu imeendelea kuwa mbaya na kusababisha madhara makubwa kiuchumi, kijamii na kiikolojia. Baadhi ya sababu zinazochangia kuathirika kwa ikolojia hii ni pamoja na kukosekana kwa usimamizi thabiti na jumuishi wa rasilimali za maji, ongezeko la shughuli za kilimo na ufugaji usiozingatia utaalamu, mabadiliko ya tabianchi, kukosekana kwa mipango ya matumizi ya ardhi, na ukosefu wa elimu ya matumizi endelevu ya maliasili.

Baada ya tafakari ya kina ya hali hii na kwa kuzingatia umuhimu wa eneo hili, ofisi yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeona kuna haja ya kuwa na mtazamo mpya wa namna ya kukabiliana na changamoto za Bonde la Mto Ruaha Mkuu kwa ufanisi zaidi. Hivyo basi, kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, Ofisi yangu iliunda Kikosi Kazi cha Kitaifa cha kunusuru ikolojia ya bonde la Mto Ruaha Mkuu kinachojumuisha viongozi, watendaji na wataalam katika sekta muhimu. Kikosi kazi hiki kilikuwa na jukumu la kuandaa mtazamo mpya wa kukabiliana na changamoto hizo, ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za haraka na za dharura na kubuni mikakati, mipango na mbinu bora zaidi za kukabiliana na changamoto za Mto Ruaha Mkuu. Kikosi Kazi hiko nilikizindua rasmi tarehe 11 Aprili, 2017, mjini Iringa.

Ni kwa muktadha huu, ninaagiza na kuwataka wadau wote kushiriki ipasavyo katika utekelezaji wa Mpango kazi wa kuokoa mfumo-ikolojia wa bonde la Mto Ruaha Mkuu ili kuhakikisha kuwa mazingira na mifumo ikolojia ya bonde la mto Ruaha Mkuu yanarudia katika hali ya awali ili kutoa huduma inayostahili kwa jamii na nchi kwa ujumla kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho.

………………………………………………….

**Mhe. Samia Suluhu Hassan**
**MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

## YALIYOMO


**ORODHA YA VIFUPISHO** ..... i

**DIBAJI** ..... ii

**TAMKO LA MHE. MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KUHUSU RASIMU YA MPANGO WA KUHIFADHI IKOLOJIA YA MTO RUAHA MKUU** ..... iii

**1.0 Utangulizi** ..... 1
**1.2 Lengo la Mpango** ..... 1
**1.3 Umuhimu wa kuwepo kwa mpango** ..... 1
**1.4 Mpangilio wa mpango** ..... 2

**2.0 HALI HALISI YA BONDE LA MTO RUAHA MKUU** ..... 2
**2.1 Umuhimu wa Bonde na uharibifu wa mazingira** ..... 2
**2.2 Juhudi za Usimamizi wa Mazingira** ..... 2
**2.3 Masuala muhimu yaliyozingatiwa katika Mpango** ..... 3
**2.3.1 Masuala muhimu ya Kisera na Kisheria** ..... 3
**2.3.2 Masuala muhimu ya Kimkakati** ..... 4
2.3.3 Masuala muhimu ya Kiutendaji ..... 5

**3.0 MPANGO** ..... 0
**3.1 Maeneo ya utekelezaji** ..... 0
**3.1.1 Usimamizi wa Matumizi Endelevu ya Rasilimali Maji** ..... 9
Lengo ..... 9
Umuhimu ..... 9
Mikakati ..... 9
Shabaha ..... 9
Viashiria ..... 10
**3.1.2 Kuimarisha upatikanaji, Matumizi na Usimamizi endelevu wa Rasilimali Ardhi** ..... 11
**Lengo** ..... 11
Uhalali ..... 11
Mikakati ..... 11
Shabaha ..... 11
Viashiria ..... 11
**3.1.3 Kuimarisha Usimamizi endelelevu wa Mazingira, Hifadhi za Taifa na Misitu** ..... 12
**Lengo** ..... 12
**Uhalali** ..... 12
Mikakati ..... 12
Shabaha ..... 12
Viashiria ..... 12
**3.1.4 Kusimamia shughuli endelevu za uzalishaji katika sekta za Nishati, Kilimo, Ufugaji, Uvuvi na Shughuli za Kijamii** ..... 13
Lengo ..... 13
Uhalali ..... 13
Mikakati ..... 13
**Shabaha** ..... 13
**Viashiria** ..... 13

**Lengo** ..... 13
Uhalali ..... 13
Mikakati ..... 13
**Shabaha** ..... 13
**Viashiria** ..... 14
**Lengo** ..... 14
Uhalali ..... 14
Mikakati ..... 14
**Viashiria** ..... 14
**Viashiria** ..... 14
**3.1.5 Kuanzisha na KuimarishaTaasisi na Mifuko inayosimamia maendeleo ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu** ..... **15**
Lengo ..... 15
Uhalali ..... 15
Mikakati ..... 15
Shabaha ..... 15
Viashiria ..... 15
**3.1.6 Kupitia na Kuboresha utekelezaji wa Sera na Sheria zinazohusu Usimamizi wa Bonde la Mto Ruaha Mkuu** ..... **15**
Lengo ..... 15
Uhalali ..... 16
Mkakati ..... 16
Shabaha ..... 16
Kiashiria ..... 16
**3.1.7 Kuboresha uratibu wa shughuli za usimamizi wa Bonde la Mto Ruaha Mkuu.** ..... **16**
Lengo ..... 16
Uhalali ..... 16
Mikakati ..... 16
Shabaha ..... 17
Viashiria ..... 17
**Majedwali ya Mpango Kazi: Rasimu ya Mpango kazi wa Kitaifa wa Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu** ..... **18**
**4.0 MAENEO MUHIMU YA KIPAUMBELE** ..... **63**
**KIAMBATISHI NAMBA 1** ..... **66**

## 1.0 Utangulizi

Bonde la Mto Ruaha Mkuu ni moja ya mabonde manne yanayounda Bonde la Rufiji. Mabonde mengine ni Kilombero, Luwegu na Rufiji chini. Bonde hili lina ukubwa wa kilometa za mraba 85,554 ambazo ni sawa na asilimia 47 ya eneo lote la Bonde la Rufiji. Bonde la Mto Ruaha Mkuu ni muhimu sana kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa maendeleo ya taifa letu. Miongoni mwa utajiri wa asili kwenye bonde hili ni pamoja na ardhi oevu ya Usangu yenye ustawi wa bioanuai na uhakika wa upatikanaji wa maji kwa jamii katika ukanda wa chini hasa mabwawa ya Mtera na Kidatu ambayo hufua umeme kwa kutumia maporomoko ya maji. Vile vile, bonde hili ni muhimu kwa shughuli za kilimo na ufugaji, uvuvi, utalii, usafirishaji na uchakataji wa mazao ya chakula. Kutokana na umuhimu huo, Serikali na wadau mbalimbali wamekuwa wakifanya jitahada za kutunza Mazingira ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi endelevu ya rasilimali zilizopo kwenye bonde.

Pamoja na jitihada hizo, hali ya ikolojia ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu imeendelea kuwa mbaya na kusababisha madhara makubwa kiuchumi, kijamii na kiikolojia. Baadhi ya sababu zinazochangia kuathirika kwa ikolojia hii ni pamoja na kukosekana kwa usimamizi thabiti na jumuishi wa rasilimali za maji, ongezeko la idadi ya watu hususan wahamiaji, ongezeko la shughuli za kilimo na ufugaji usiozingatia utaalamu, mabadiliko ya tabianchi, kukosekana kwa matumizi bora ya ardhi, udhaifu katika usimamizi wa sheria mbalimbali, ukosefu wa elimu ya matumizi endelevu ya maliasili, na kutokutekelezwa kwa baadhi ya matamko na maagizo muhimu yaliyotolewa na viongozi wa kisiasa. Hali hii imepelekea Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo mwezi Aprili 2017 kuunda kikosi kazi cha kitaifa kwa lengo la kufanya tathmini ya ukubwa wa tatizo, juhudi zilizofanyika, kupokea maoni ya wadau, kutoa mapendekezo kuhusu hatua za kuchukua na kuandaa mpango wa kusimamia mazingira ya bonde hilo pamoja na mpango kazi wa utekelezaji.

### *1.2 Lengo la Mpango*

Mpango huu unatoa mwongozo wa namna ya kusimamia mazingira ya bonde na kutekeleza mapendekezo ya kikosi kazi katika kurejesha ikoloji ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu. Mpango huu umeainisha maeneo muhimu ya utekelezaji, mikakati ya utekelezaji, wadau na wahusika muhimu, muda wa utekelezaji, matokeo tarajiwa na viashiria vya matokeo.

Aidha, uchambuzi wa gharama za utekelezaji wa mpango utafanyika baada ya kuwashirikisha wadau watakaotekeleza mpango huu.

### *1.3 Umuhimu wa kuwepo kwa mpango*

Ili kufaniksiha utekelezaji wa mapendekezo ya kikosi kazi, ni muhimu kuandaa mpango thabiti unaoonyesha namna ya kutekeleza mapendekezo yaliyotajwa kwenye taarifa ya kikosi kazi. Shughuli zilizoainishwa kwenye Mpango zimeelekezwa moja kwa moja kwa muhusika Mkuu akisaidiana na wadau wengine ili kuimarisha usimamizi wa pamoja.

*1.4 Mpangilio wa mpango*

Mpango huu umegawanyika katika sehemu tatu zifuatazo:-

- Sehemu ya kwanza ni utangulizi ambao unaeleza chimbuko la kuwepo kwa mpango, ukubwa wa tatizo, juhudi zilichofanyika, lengo na uhalali wa kuwepo kwa mpango na mpangilio wa sura mbalimbali katika andiko la mpango;
- Sehemu ya pili inaeleza hali halisi ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu zikiwemo fursa za maendeleo ya uchumi na ustawi wa jamii, pamoja na changamoto zinazolikabili bonde hilo; na
- Sehemu ya tatu inaonesha maeneo ya utekelezaji, sababu za utekelezaji wa kila eneo, mikakati ya utekelezaji pamoja na matokeo tarajiwa katika kila eneo la utekelezaji.

## 2.0 HALI HALISI YA BONDE LA MTO RUAHA MKUU

*2.1 Umuhimu wa Bonde na uharibifu wa mazingira*

Bonde la Mto Ruaha Mkuu lina fursa nyingi za maendeleo ya kiuchumi na kijamii kama vile kilimo cha umwagiliaji, malisho ya mifugo, uvuvi, hifadhi za misitu, hifadhi za wanyamapori pamoja na uzalishaji wa umeme. Maeneo ya umwagiliaji hususan, katika eneo la Usangu yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka kutoka hekta 14,000 mwaka 1980 mpaka hekta 24,000 mwaka 1990 na kufikia hekta za mraba 115,000 mwaka 201, hali inayochangia kupungua kwa mtiririko wa maji katika Mto Ruaha Mkuu mwaka hadi mwaka. Hii inaonyesha kwamba, kilimo cha umwagiliaji ndio tegemeo pekee la kipato na maisha ya kujikimu ya wananchi wa bonde hili. Kimfumo, bonde la Mto Ruaha Mkuu lina mtandao imara wa wadau wa sekta ya umma wakishirikiana na sekta binafsi katika kutatua changamoto mbalimbali za kimaendeleo ikiwemo utunzaji wa Mto Ruaha Mkuu.

Bonde la Mto Ruaha Mkuu linakabiliwa na uharibifu mkubwa wa mazingira hususan, kwenye vyanzo vya maji. Uharibifu huu unatokana na shughuli za kibinadamu zisizo endelevu zinazofanyika kwenye vilele vya milima, miteremko ya milima na katika ardhi oevu. Sababu nyingine ni kukosekana kwa usimamizi thabiti wa rasilimali za maji, ongezeko la idadi ya watu, ongezeko la shughuli za kilimo cha umwagiliaji na ufugaji, mabadiliko ya tabianchi, kukosekana kwa matumizi bora ya ardhi, udhaifu katika usimamizi wa sheria mbalimbali, ukosefu wa elimu ya matumizi endelevu ya maliasili na kutotekelezwa kwa matamko na maagizo ya viongozi wa kisiasa. Vile vile kuna uratibu hafifu wa wadau wanaofanya kazi zao katika bonde la Mto Ruaha Mkuu hali iliyosababisha kuongezeka kwa changamoto za utunzaji wa mazingira ya bonde.

Historia inaonesha kwamba kabla ya miaka ya 1980 mtiririko wa maji katika Mto Ruaha Mkuu wakati wa kiangazi ulikuwa kati ya mita za ujazo 0.5 – 1.0 kwa sekunde. Uharibifu wa mazingira na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu, hasa kilimo cha umwagiliaji kisicho endelevu, ufugaji, upandaji wa miti ya kibiashara na uvunaji wa misitu usio endelevu na shughuli nyingine za kibinadamu zimesababisha mtiririko wa maji katika mito na vijito kupungua na kukauka kwa muda mrefu kuliko ilivyokuwa hapo awali.

### 2.2 Juhudi za Usimamizi wa Mazingira

Serikali na wadau mbalimbali wamekuwa wakitekeleza shughuli za utunzaji wa mazingira ya bonde la Mto Ruaha Mkuu kwa kuzingatia miongozo ya Sera na Sheria mbalimbali ili kuhuisha ikolojia ya bonde. Aidha, kumekuwa na program na miradi mbalimbali ambayo imekuwa ikitekelezwa katika bonde la Mto Ruaha Mkuu kwa lengo hilo hilo.

Pamoja na juhudi zilizofanyika, hali ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu imeendelea kuwa mbaya na kutishia maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kiikolojia.

*2.3 Masuala muhimu yaliyozingatiwa katika Mpango*

Kwa kuzingatia uchambuzi wa hali halisi ya bonde la Mto Ruaha Mkuu, miongoni mwa mambo yaliyozingatiwa ni pamoja na taarifa zinazotokana na mapendekezo 30 ya taarifa ya kikosi kazi yaliyopendekezwa kwa kuzingatia masuala ya kisera na kisheria, kimkakati na kiutendaji kama ifuatavyo: -

*2.3.1 Masuala muhimu ya Kisera na Kisheria*

(i) Serikali iunde **Mamlaka Maalum** kisheria itakayokuwa na jukumu la kusimamia matumizi endelevu ya raslimali zilizopo katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu. Pamoja na mamlaka hiyo uundwe **Mfuko Maalum** wa Wakfu ***(Trust Fund)*** ambao **utachangiwa na wote wanaonufaika na rasilimali za Bonde** na wadau wengine na usimamiwe kwa pamoja na wadau hao (Serikali, sekta binafsi na wabia wa Bonde la Mto Rufiji). Taasisi hiyo iwe chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Aidha, ili kutekeleza pendekezo hilo mpango uhusishe hatua mbili kuu (i) kwa kuanzia Mamlaka hiyo ianzishwe kwa kutumia **Sheria ya Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 kwa maana ya Eneo Lindwa *(Environmentally Protected Area)*** na (ii) Baadaye itolewe sheria maalum ya kuunda Mamlaka, Mfuko na utaratibu wa kuuchangia na kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za Bonde.

Kikosi Kazi kinatambua zipo mamlaka mbalimbali ambazo zimeundwa katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu/Rufiji hivyo, ufanyike mpango wa **kurazinisha** mipaka na majukumu ya mamlaka hizo ili ziweze kutekeleza majukumu yake chini ya Mamlaka Maalum na Mfuko.

(ii) Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi wahakikishe Wilaya na Vijiji vyote vilivyopo ndani ya Bonde vinaandaa, kutekeleza na kusimamia **Mipango ya Matumizi ya Ardhi.** Aidha, mipango iliyopo ipitiwe na kuhuishwa.

(iii) Ili kuhakikisha **wamiliki wa ardhi wanatumia rasilimali hiyo kwa uendelevu utakaochangia utunzaji wa ikolojia ya Bonde,** Ofisi ya Rais TAMISEMI, Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi ziharakishe **uwekaji wa ukomo wa kiwango cha juu cha ardhi** ambacho kinaweza kumilikiwa na kutumiwa kwa kilimo, misitu, ufugaji, viwanda, makazi na matumizi mengine kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999.

(iv) Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Maji na Umwagiliaji ziharakishe kubainisha vyanzo vya maji katika Bonde hususan, milima, na misitu ya asili na kuondoa shughuli za kibinadamu. Aidha, vyanzo vyote vya maji ndani ya bonde, vipimwe na

viwekewe mipaka kwa kutumia alama zinazoonekana kwa urahisi; na kumilikishwa kwa mamlaka husika. Mfano mzuri upo katika Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi-TANROADS katika kuweka mipaka ya maeneo ya barabara.

(v) Ofisi ya Makamu wa Rais isimamie uandaaji wa SEA katika Bonde. Katika kuandaa SEA hiyo, wadau wote washirikishwe. Aidha, Sera na Sheria ya Mazingira pamoja na Sera na Sheria nyingine zinazohusika katika eneo hilo zitazamwe upya.

(vi) Ofisi ya Rais TAMISEMI ikishirikiana na Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Fedha na Mipango iandae utaratibu wa kutoza kodi ya mifugo. Mapato yatakayotokana na kodi hiyo yalenge kuipatia Serikali uwezo wa kuboresha tija na uzalishaji katika sekta ya mifugo hususan ujenzi wa miundombinu, masoko, nyanda za malisho na ujenzi wa viwanda vya chakula cha mifugo kwa kushirikiana na sekta binafsi.

(vii) Ofisi ya Makamu wa Rais, ihakikishe Wizara za kisekta zinasimamia Sera na Sheria katika utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii katika Bonde. Mamlaka inayopendekezwa ipewe uwezo wa kuhakikisha kazi zote zinazotekelezwa katika Bonde zinazingatia Sera na Sheria zilizopo za uhifadhi wa mazingira na ikolojia ya Bonde.

(viii) Wizara za kisekta zikishirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria zifanye mapitio ya sera na sheria za sekta zinazohusika moja kwa moja katika utunzaji wa mazingira ya Bonde na nchini kwa ujumla ili kuhakikisha zina uwezo wa kuwezesha wadau kusimamia kwa ufanisi zaidi matumizi endelevu ya raslimali za Bonde na mazingira kwa ujumla.

(ix) Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi ikishirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria iandae utaratibu wa kupatikana kwa sheria ya ujumla inayosimamia ardhi na raslimali za sekta ya kilimo.

(x) Kutokana na umuhimu wa misitu ya biashara kwa ustawi wa wananchi katika maeneo ya Bonde, taasisi za utafiti wa mbegu za misitu zizalishe mbegu za miti ya biashara isiyotumia maji kwa wingi.

(xi) Kwa kuwa rasilimali maji ni muhimu sana kwa uhai na ina wadau wengi, ipo haja ya kuanzishwa kwa **"Water Resource Regulatory Authority"** ambayo itadhibiti matumizi ya maji nchini. Wizara ya Maji na Umwagiliaji wamepewa majukumu ya kuhakikisha kila Mtanzania anapata maji safi na salama ya kunywa; Sekta ya Kilimo inahitaji maji kwa ajili ya umwagiliaji (irrigation); Sekta ya Mifugo inahitaji maji kwa ajili ya mifugo; Uvuvi vile vile inahitaji maji kwa ajili ya shughuli za uvuvi na ufugaji wa samaki na kila sekta inahitaji maji kwa ajili ya matumizi mbali mbali, hivyo Wizara ya Maji na Umwagiliaji ni mdau mmojawapo na hawezi kuwa sehemu ya mtoa vibali vya kutumia maji kwa sekta nyingine.

*2.3.2 Masuala muhimu ya Kimkakati*

(i) Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi ihakikishe uzalishaji wa mazao, mifugo na uvuvi unafanyika kwa kutumia mbinu bora za uzalishaji. Uzalishaji wa mazao ya kilimo uzingatie **kilimo hifadhi** katika maeneo yanayotegemea mvua na **kilimo shadidi** katika maeneo ya umwagiliaji; ufugaji uzingatie uwezo wa maeneo ya malisho (carrying capacity) na uboreshaji na utunzaji wa nyanda za malisho. Aidha, uendelezaji wa uvuvi na ufugaji wa samaki kwenye mito na mabwawa na maeneo oevu usimamiwe ili ufanyike katika taratibu endelevu. Kazi hii iendane

na utengaji wa maeneo ya uwekezaji wa miundombinu ya kuongeza thamani na masoko ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

(ii) Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi iharakishe kukamilisha kazi inayoendelea ya utambuzi na uwekaji alama mifugo yote. Kazi hii iendane na kazi inayoendelea ya utengaji wa maeneo ya malisho na uwekaji wa miundombinu ya mifugo (majosho, njia za mifugo, mabirika ya kunyweshea mifugo, minada, viwanda vya vyakula vya mifugo na kuchakata mazao ya mifugo).

(iii) Mamlaka inayopendekezwa ihakikishe mipango na shughuli za sekta mbalimbali ndani ya Bonde inaratibiwa ili kuhakikisha inatekelezwa kwa utaratibu endelevu na inachangia katika maslahi mapana ya maendeleo ya Bonde badala ya kila taasisi na mipango yake.

(iv) Ofisi ya Makamu wa Rais ihakikishe miradi yote inayotekelezwa ndani ya Bonde ambayo haijafanyiwa EIA ifanyiwe.

(v) Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, ihakikishe taasisi zote zinazosimamia utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii katika Bonde zinatoa elimu kuhusu mbinu za kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

2.3.3 Masuala muhimu ya Kiutendaji

(i) Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali waharakishe utekelezaji wa **Tangazo la Serikali Na. 28 la mwaka 2008** kwa kuzingatia sheria na taratibu. Tangazo hilo linahusu kupandisha hadhi eneo la Usangu kuwa sehemu ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

(ii) Ili kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali maji katika eneo la Bonde yanakidhi mahitaji ya wadau wote, Mamlaka inayopendekezwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Maji na Umwagiliaji zihakikishe kilimo cha umwagiliaji kinaboreshwa na kutekelezwa kulingana na sheria na taratibu zilizopo. Aidha, ifanyike tathmini ya kiasi cha maji katika kila chanzo, mahitaji katika skimu za umwagiliaji zilizopo kwa sasa na kulinganishwa na vibali vilivyotolewa. Teknolojia za kisasa zitumike katika kuongeza ufanisi katika miradi ya umwagiliaji. Serikali ihakikishe wawekezaji wote wapya katika bonde wanatumia teknolojia zinazohifadhi maji. Aidha, skimu za mashamba makubwa zilizopo zibadilishwe kwenda kwenye mfumo unaotumia maji machache.

(iii) Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikana na Wizara ya Maliasili na Utalii ifanye tathmini ya kina kwa ajili ya kutambua maeneo yanayopaswa kubakizwa katika uoto wa asili na misitu ya asili na yale yanayoweza kutumika kwa upandaji wa miti isiyo ya asili kibiashara bila kuathiri ikolojia na upatikanaji wa maji. Pale ambapo tathmini itabaini miti isiyo ya asili inaathiri mazingira, miti hiyo iondolewe. Aidha, tathmini hiyo ielekeze upandaji wa miti kibiashara ufanyike kwa kuzingatia mipango ya matumizi ya ardhi.

(iv) Ofisi ya Rais TAMISEMI ikishirikiana na Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi ihakikishe kilimo katika maeneo ya miteremko/mwinamo yanajengewa makinga-maji, kubakiza uoto wa asili na kilimo hifadhi na kutumia mbinu nyingine za kuzuia mmomonyoko wa

udongo. Aidha, tathmini ifanyike kubaini maeneo yasiyofaa kwa kilimo kutokana na mitelemko mikali, ili maeneo hayo yazuiliwe kutumika kwa kilimo na makazi.

(v) Wizara ya Maji na Umwagiliaji ifanye tathmini ya maeneo ambayo mito imepoteza muelekeo na kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mpango wa kurejesha mito hiyo katika mikondo yake. Aidha, Wizara isimamie ukamilishaji wa kazi iliyoanza katika baadhi ya mito ya Ndembera, Mswiswi, Mkoji na Kioga.

(vi) Wizara ya Maji na Umwagiliaji ihakikishe uwekaji wa vipimo vya maji *(flow meters)* unafanyika katika mabanio na matupio ya maji ili kujua kiasi cha maji kinachotumika na kinachorudishwa mtoni kulingana na kibali cha maji kilichotolewa. Watumiaji wa skimu zote za umwagiliaji ambazo hazina vipimo waweke vipimo vya kujua kiasi cha maji kinachochukuliwa na kurudishwa mtoni. Aidha, wamiliki wa mashamba ya umwagiliaji ambao hawajafunga vipimo hivyo wasitishiwe vibali.

(vii) Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe kuwa kilimo kisichozingatia kilimo hifadhi na kilimo shadidi kinasitishwa katika eneo la Bonde la Mto Ruaha Mkuu. Aidha, kutokana na ukubwa wa kazi hiyo utolewe muda wa kutoa elimu kwa Watendaji ili watumike kuelimisha wakulima juu utekelezaji wa kilimo hicho.

(viii) Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi zifanye tathmini kwa ajili ya kujenga mabwawa ya kuvuna maji ya mvua ili yasaidie kuwepo na mtiririko wa maji kwa mwaka mzima na kutumika kwa shughuli za kiuchumi na kijamii. Mabwawa makubwa yaliyopendekezwa ya uvunaji wa maji ya mvua ya Ndembera na Usalimwani yajengwe na Bwawa la Lwanyo ujenzi ukamilike.

(ix) Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara Ardhi Nyumba na Mandeleo ya Makazi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji zifanye uhakiki wa milki zote zilizotolewa katika ardhi oevu na vyanzo vya maji katika eneo la Bonde ili zibatilishwe.

(x) Ofisi ya Rais TAMISEMI ikishirikiana na wadau isimamie utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi iliyopo katika Bonde kwa kuzingatia mapendekezo na mpango kazi wa Kamati ya Kisekta ya Utatuzi wa Migogoro ya Matumizi ya Ardhi iliyoundwa na Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Serikali itoe kipaumbele kwa utekelezaji wa mpango wa ***Kupanga-Kupima-Kumilikisha (K3)*** eneo lote la ardhi katika Bonde.

(xi) Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Nishati na Madini na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira zifanye tathmini ya maeneo ya uchimbaji wa madini katika bonde kwa lengo la kutambua uchimbaji unaofanyika katika vyanzo vya maji na maeneo oevu na kuusitisha. Vilevile, Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Bonde zitunge sheria ndogo zinazowataka wachimbaji wa madini ya aina zote katika maeneo ya Bonde kupata kibali cha uchimbaji. Aidha, Wizara ya Nishati na Madini isitoe leseni za uchimbaji wa madini katika Bonde bila kuzishirikisha Halmashauri husika.

(xii) Ofisi ya Makamu wa Rais, ihakikishe huduma za ukaguzi na 'Ufuatiliaji na Tathmini' zinatolewa na Ofisi za Kanda za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Aidha, Wizara ya Maji na Umwagiliaji ihakikishe Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Bodi ya Maji ya Bonde zinaimarishwa na kuratibiwa ipasavyo.

(xiii) Ofisi ya Makamu wa Rais iandae mfumo utakaohakikisha kuwa sehemu ya mchango wa wadau wanaotumia raslimali maji katika Bonde inatumika kuchangia miradi ya maendeleo ya wananchi kama sehemu ya hamasa ya utunzaji wa vyanzo vya maji. Aidha Ofisi, ihakikishe taasisi zinazonufaika kutokana na huduma za upatikanaji wa maji zinabuni utaratibu wa kufikisha huduma za jamii kwa unafuu.

(xiv) Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi pamoja na wadau wengine itekeleze mpango maalum wa kuwawezesha wakazi wa Bonde kuanzisha na kutekeleza shughuli mbadala za kiuchumi ambazo ni rafiki kwa mazingira.

(xv) Kikosi Kazi kinapendekeza Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maliasili na Utalii wahakikishe kuwa mifugo yote iliyopo katika maeneo ya Hifadhi za Taifa, Hifadhi za Akiba na maeneo mengine yaliyoanishwa kwa shughuli zisizo za ufugaji inaondolewa haraka.

(xvi) Wizara ya Maji na Umwagiliaji ikishirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango ziharakishe utekelezaji wa Mfuko wa Umwagiliaji kupitia ukusanyaji wa maduhuli kama fidia ya uwekezaji uliofanyika katika miradi ya umwagiliaji ili mapato hayo yatumike katika kuboresha miundombinu ya umwagiliaji katika skimu zilizopo na ujenzi wa skimu mpya.

(xvii) Watu wote waliokiuka taratibu watambuliwe na wachukuliwe hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kutozwa faini kulingana na taratibu na sheria. Aidha, wale wote waliotambuliwa na Kikosi Kazi na kutozwa faini wafuatiliwe ili kuhakikisha wote wanalipa faini hizo. Kikosi Kazi kilibaini wakiukaji wa sheria katika Bonde wapatao 11 ambao walitozwa faini ya jumla ya Shilingi milioni 224,490,000/=.

(xviii) Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Ofisi ya Rais –TAMISEMI wafuatilie na kumaliza mgogoro wa mpaka kati ya skimu ya Igomelo na Hifadhi ya Akiba ya Mpanga-Kipengere. Kikosi kazi kinashauri, banio la skimu ya Igomelo libaki ndani ya Hifadhi ila eneo lote la skimu libaki kwa wananchi kama sehemu ya utatuzi wa mgogoro huo.

(xix) Kutokana na ongezeko kubwa la watu katika bonde, kuwepo na hatua za kudhibiti ongezeko la watu kwa kutoa elimu ya idadi ya watu kuwiana na matumizi endelevu ya raslimali za asili.

(xx) Jitihada zielekezwe katika kuongeza uzalishaji (productivity) badala ya kuongeza maeneo yanayolimwa.

## 3.0 MPANGO

Mpango wa Kitaifa wa hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu ni mpango unaolenga kuratibu usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, ardhi na rasilimali zinazohusiana nazo, ili kupata matokeo mazuri zaidi ya kiuchumi na kijamii katika uwiano sawa pasipo kuathiri uendelevu wa mfumo wa ikolojia kwa manufaa ya kizazi cha sasa na baadaye.

Mpango huu unategemea kutekelezwa kama ulivyopangwa na kufikia malengo yaliyowekwa, hata hivyo vihatarishi mbalimbali ambavyo vimebainishwa kwenye kiambatisho namba 1 vinaweza kwa namna moja au nyingine kuchelewesha au kukwamisha utekelezaji wa mpango huu.

### *3.1 Maeneo ya utekelezaji*

Mpango umependekeza maeneo makuu saba ambayo yatapelekea kuhuishwa kwa mifumo ikolojia na ustawi wa bioanuai endelevu kwa ajili ya jamii, uchumi na mazingira. Maeneo haya yanatokana na mapendekezo 36 yaliyobainishwa katika taarifa ya Kikosi Kazi (Jedwali namba 1) na kutafsiriwa katika mikakati na shughuli mbalimbali. Maeneo ya utekelezaji yaliyopendekezwa ni yafuatayo: -

i. Kuanzisha na KuimarishaTaasisi na Mfuko inayosimamia maendeleo ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu;
ii. Kuimarisha upatikanaji, matumizi na usimamizi endelevu wa rasilimali Ardhi;
iii. Kuboresha, upatikanaji, matumizi na usimamizi endelevu wa rasilimali za maji;
iv. Kuimarisha usimamizi endelevu wa Mazingira, Hifadhi za Taifa na Misitu;
v. Kupitia na Kuboresha utekelezaji wa Sera na Sheria zinazohusu Usimamizi wa Bonde la Mto Ruaha Mkuu;
vi. Kusimamia shughuli endelevu za Nishati, Uhifadhi, Kilimo, Ufugaji, Uvuvi na Shughuli za Kijamii; na
vii. Kuboresha uratibu wa Shughuli za usimamizi wa Bonde la Mto Ruaha Mkuu.

**Jedwali Namba 1: Maeneo saba ya utekelezaji yatokanayo na mapendekezo ya taarifa ya kikosi kazi**

| Maeneo ya Utekelezaji | Mapendekezo ya Kikosi kazi |
|---|---|
| 1.0 Kuboresha upatikanaji, matumizi na usimamizi endelevu wa Rasilimali Maji | 1.1 **Mapendekezo ya Kisera na Kisheria**<br><br>1.1.1 Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Maji na Umwagiliaji ziharakishe kubainisha vyanzo vya maji katika Bonde hususan, milima, na misitu ya asili na kuondoa shughuli za kibinadamu. Aidha, vyanzo vyote vya maji ndani ya bonde, vipimwe na viwekewe mipaka kwa kutumia alama zinazoonekana kwa urahisi; na kumilikishwa kwa mamlaka husika. Mfano mzuri upo katika Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi-TANROADS katika kuweka mipaka ya maeneo ya barabara.<br><br>1.1.2 Kwa kuwa rasilimali maji ni muhimu sana kwa uhai na ina wadau wengi, upo umuhimu wa kuanzishwa kwa "**Water Resource Regulatory Authority**" ambayo itadhibiti matumizi ya maji nchini. Wizara ya Maji na Umwagiliaji imepewa majukumu ya kuhakikisha kila Mtanzania anapata maji safi na salama ya kunywa; Sekta ya Kilimo inahitaji maji kwa ajili ya umwagiliaji (irrigation); Sekta ya Mifugo inahitaji maji kwa ajili ya mifugo; Uvuvi vile vile inahitaji maji kwa ajili ya uvuvi na kila sekta inahitaji maji kwa ajili ya matumizi mbali mbali hivyo, Wizara ya Maji na Umwagiliaji ni mdau mmojawapo na hawezi kuwa sehemu ya mtoa vibali vya kutumia maji kwa sekta nyingine. |
| | **1.2 Mapendekezo ya Kiutendaji**<br><br>1.2.1 Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali waharakishe utekelezaji wa **Notisi ya Serikali Na. 28 ya mwaka 2008** kwa kuzingatia sheria na taratibu. Notisi hiyo inahusu kupandisha hadhi eneo la Usangu kuwa sehemu ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.<br><br>1.2.2 Ili kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali maji katika eneo la Bonde yanakidhi mahitaji ya wadau wote, Mamlaka inayopendekezwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Wizara ya Maji na Umwagiliaji zihakikishe kilimo cha umwagiliaji kinaboreshwa na kutekelezwa kulingana na sheria na taratibu zilizopo. |

| | |
|---|---|
| | Aidha, ifanyike tathmini ya kiasi cha maji katika kila chanzo, mahitaji katika skimu za umwagiliaji zilizopo kwa sasa na kulinganishwa na vibali vilivyotolewa. Teknolojia za kisasa zitumike katika kuongeza ufanisi katika miradi ya umwagiliaji. Serikali ihakikishe wawekezaji wote wapya katika bonde wanatumia teknolojia zinazohifadhi maji. Aidha, skimu za mashamba makubwa zilizopo zibadilishwe kwenda kwenye mfumo unaotumia maji machache.<br><br>1.2.3 Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikana na Wizara ya Maliasili na Utalii ifanye tathmini ya kina kwa ajili ya kutambua maeneo yanayopaswa kubakizwa katika uoto wa asili na misitu ya asili na yale yanayoweza kutumika kwa upandaji wa miti isiyo ya asili kibiashara bila kuathiri ikolojia na upatikanaji wa maji. Pale ambapo tathmini itabaini miti isiyo ya asili inaathiri mazingira, miti hiyo iondolewe. Aidha, tathmini hiyo ielekeze upandaji wa miti kibiashara ufanyike kwa kuzingatia mipango ya matumizi ya ardhi.<br><br>1.2.4 Wizara ya Maji na Umwagiliaji ifanye tathmini ya maeneo ambayo mito imepoteza muelekeo na kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mpango wa kurejesha mito hiyo katika mikondo yake. Aidha, Wizara isimamie ukamilishaji wa kazi iliyoanza katika baadhi ya mito ya Ndembera, Mswiswi, Mkoji na Kioga.<br><br>1.2.5 Wizara ya Maji na Umwagiliaji ihakikishe uwekaji wa vipimo vya maji (*flow meters*) unafanyika katika mabanio na matupio ya maji ili kujua kiasi cha maji kinachotumika na kinachorudishwa mtoni kulingana na kibali cha maji kilichotolewa. Watumiaji wa skimu zote za umwagiliaji ambazo hazina vipimo waweke vipimo vyakujua kiasi cha maji kinachochukuliwa na kurudishwa mtoni. Aidha, wamiliki wa mashamba ya umwagiliaji ambao hawajafunga vipimo hivyo wasitishiwe vibali.<br><br>1.2.6 Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi zifanye tathmini kwa ajili ya kujenga mabwawa ya kuvuna maji ya mvua ili yasaidie kuwepo na mtiririko wa maji kwa mwaka mzima na kutumika kwa shughuli za kiuchumi na kijamii. Mabwawa makubwa yaliyopendekezwa ya uvunaji wa maji ya mvua ya Ndembera na Usalimwani yajengwe na la Bwawa la Lwanyo ujenzi ukamilike.<br><br>1.2.7 Wizara ya Maji na Umwagiliaji ikishirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango ziharakishe utekelezaji wa Mfuko wa Umwagiliaji kupitia ukusanyaji wa maduhuli kama fidia ya uwekezaji uliofanyika katika miradi ya |

| | |
|---|---|
| | umwagiliaji ili mapato hayo yatumike katika kuboresha miundombinu ya umwagiliaji katika skimu zilizopo na ujenzi wa skimu mpya. |
| 2.0 Kuimarisha upatikanaji, Matumizi na Usimamizi endelevu wa Rasilimali Ardhi | 2.1 **Mapendekezo ya Kisera na Kisheria**<br><br>2.1.1 Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi wahakikishe Wilaya na Vijiji vyote vilivyopo ndani ya Bonde Vinaandaa, kutekeleza na kusimamia Mipango ya Matumizi ya Ardhi Aidha, mipango iliyopo ipitiwe na kuhuishwa.<br><br>2.1.2 Ili kuhakikisha wamiliki wa ardhi wanatumia rasilimali hiyo kwa uendelevu utakaochangia utunzaji wa ikolojia ya Bonde, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi ziharakishe uwekaji wa ukomo wa kiwango cha juu cha ardhi ambacho kinaweza kumilikiwa na kutumiwa kwa kilimo, misitu, ufugaji, viwanda, makazi na matumizi mengine kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999.<br><br>**2.2 Mapendekezo ya Kiutendaji**<br><br>2.2.1 Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Wizara Ardhi Nyumba na Mandeleo ya Makazi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji zifanye uhakiki wa milki zote zilizotolewa katika ardhi oevu na vyanzo vya maji katika eneo la Bonde ili zibatilishwe.<br><br>2.2.2 Ofisi ya Rais-TAMISEMI ikishirikiana na wadau isimamie utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi iliyopo katika Bonde kwa kuzingatia mapendekezo na mpango kazi wa Kamati ya Kisekta ya Utatuzi wa Migogoro ya Matumizi ya Ardhi iliyoundwa na Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Serikali itoe kipaumbele kwa utekelezaji wa mpango wa Kupanga-Kupima-Kumilikisha (K3) eneo lote la ardhi katika Bonde. |
| 3.0 Kuimarisha Usimamizi endelevu wa Mazingira, Hifadhi ya Taifa na | 3.1 **Mapendekezo ya Kisera na Kisheria**<br>3.1.1 Ofisi ya Makamu wa Rais isimamie uandaaji wa SEA katika Bonde. Katika kuandaa SEA hiyo, wadau wote washirikishwe. Aidha, Sera na Sheria ya Mazingira pamoja na sera na sheria nyingine husia zinazohusika katika eneo hilo zitazamwe upya. |

| | |
|---|---|
| Misitu | 3.1.2 Kutokana na umuhimu wa misitu ya biashara kwa ustawi wa wananchi katika maeneo ya Bonde, taasisi za utafiti wa mbegu za misitu zizalishe mbegu za miti ya biashara isiyotumia maji kwa wingi. |
| | **3.2 Mapendekezo ya Kimkakati**<br><br>3.2.1 Ofisi ya Makamu wa Rais ihakikishe miradi yote inayotekelezwa ndani ya Bonde ambayo haijafanyiwa EIA ifanyiwe.<br><br>3.2.2 Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, ihakikishe taasisi zote zinazosimamia utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii katika Bonde zinatoa elimu kuhusu mbinu za kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. |
| | **3.3 Mapendekezo ya Kiutendaji**<br><br>3.3.1 Ofisi ya Makamu wa Rais, ihakikishe huduma za ukaguzi na 'Ufuatiliaji na Tathmini' zinazotolewa na Ofisi za Kanda za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Bodi ya Maji ya Bonde zinaimarishwa na kuratibiwa.<br><br>3.3.2 Ofisi ya Makamu wa Rais iandae mfumo utakaohakikisha kuwa sehemu ya mchango wa wadau wanaotumia raslimali maji katika Bonde inatumika kuchangia miradi ya maendeleo ya wananchi kama sehemu ya hamasa ya utunzaji wa vyanzo vya maji. Aidha Ofisi, ihakikishe taasisi zinazonufaika kutokana na huduma za upatikanaji wa maji zinabuni utaratibu wa kufikisha huduma za jamii kwa unafuu.<br><br>3.3.3 Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi pamoja na wadau wengine itekeleze mpango maalum wa kuwawezesha wakazi wa Bonde kuanzisha na kutekeleza shughuli mbadala za kiuchumi ambazo ni rafiki kwa mazingira.<br><br>3.3.4 Watu wote waliokiuka taratibu watambuliwe na wachukuliwe hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kutozwa faini kulingana na taratibu na sheria. Aidha wale wote waliotambuliwa na Kikosi Kazi na kutozwa faini wafuatiliwe ili kuhakikisha wote wanalipa faini hizo. Kikosi Kazi kilitoza jumla ya wakiukaji wa sheria mbalimbali katika Bonde wapatao 11 walitozwa faini ya jumla ya Shilingi milioni 224,490,000/=. |

| | |
|---|---|
| | 3.3.5 Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Ofisi ya Rais –TAMISEMI wafuatilie na kumaliza mgogoro wa mpaka kati ya skimu ya Igomelo na Hifadhi ya Akiba ya Mpanga-Kipengere. Kikosi kazi kinashauri, banio la skimu ya Igomelo libaki ndani ya Hifadhi ila eneo lote la skimu libaki kwa wananchi kama sehemu ya utatuzi wa mgogoro huu. |
| 4.0 Kusimamia shughuli endelevu za Nishati, Uhifadhi, Kilimo, Ufugaji, Uvuvi na Shughuli za Kijamii | 4.1 **Mapendekezo ya Kisera na Kisheria**<br>4.1.1 Ofisi ya Rais-TAMISEMI ikishirikiana na Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Fedha na Mipango iandae utaratibu wa kuitoza kodi ya mifugo. Mapato yatakayotokana na kodi hiyo yalenge kuipatia Serikali uwezo wa kuboresha tija na uzalishaji katika sekta ya mifugo hususan ujenzi wa miundombinu, masoko, nyanda za malisho na ujenzi wa viwanda vya cha chakula mifugo kwa kushirikiana na sekta binafsi.<br><br>4.1.2 Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi ikishirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria iandae utaratibu wa kupatikana kwa sheria ya ujumla inayosimamia ardhi na raslimali za sekta ya kilimo. |
| | **4.2 Mapendekezo ya Kimkakati**<br><br>4.2.1 Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi ihakikishe uzalishaji wa mazao, mifugo na uvuvi unafanyika kwa kutumia mbinu bora za uzalishaji (Good Agricultural Practices – GAP). Uzalishaji wa mazao ya kilimo uzingatie **kilimo hifadhi** katika maeneo yanayotegemea mvua na **kilimo shadidi** katika maeneo ya umwagiliaji; ufugaji uzingatie uwezo wa maeneo ya malisho (Carrying Capacity) na uboreshaji na utunzaji wa nyanda za malisho. Aidha, uendelezaji wa uvuvi na ufugaji wa samaki kwenye mito na mabwawa na maeneo oevu usimamiwe ili ufanyike katika taratibu endelevu. Kazi hii iendane ya utengaji wa maeneo ya uwekezaji wa miundombinu ya kuongeza thamani na masoko ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.<br><br>4.2.2 Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi iharakishe kukamilisha kazi inayoendelea ya utambuzi na uwekaji alama mifugo yote. Kazi hii iendane na kazi inayoendelea ya utengaji wa maeneo ya malisho na uwekaji wa miundombinu ya mifugo (majosho, njia za mifugo, mabirika ya kunyweshea mifugo, minada, viwanda vya vyakula vya mifugo na kuchakata mazao ya mifugo). |

| | |
|---|---|
| | **4.3 Mapendekezo ya Kiutendaji**<br><br>4.3.1 Ofisi ya Rais-TAMISEMI ikishirikiana na Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi ihakikishe kilimo katika maeneo ya miteremko/mwinamo yanajengewa makinga-maji, kubakiza uoto wa asili na kilimo hifadhi na kutumia mbinu nyingine za kuzuia mmomonyoko wa udongo. Aidha, tathmini ifanyike kubaini maeneo yasiyofaa kwa kilimo kutokana na mitelemko mikali, ili maeneo hayo yazuiliwe kutumika kwa kilimo na makazi.<br><br>4.3.2 Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe kuwa kilimo kisichozingatia kilimo hifadhi na kilimo shadidi kinasitishwa katika eneo la Bonde la Mto Ruaha Mkuu. Aidha, kutokana na ukubwa wa kazi hiyo utolewe muda wa kutoa elimu kwa Watendaji ili watumike kuelimisha wakulima juu utekelezaji wa kilimo hicho.<br>4.3.3 Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Nishati na Madini na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira zifanye tathmini ya maeneo ya uchimbaji wa madini katika bonde kwa lengo la kutambua uchimbaji unaofanyika katika vyanzo vya maji na maeneo oevu na kuusitisha. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Bonde zitunge sheria ndogo zinazowataka wachimbaji wa madini ya aina zote katika maeneo ya Bonde kupata kibali cha uchimbaji. Aidha, Wizara ya Nishati na Madini isitoe leseni za uchimbaji wa madini katika Bonde bila kuzishirikisha Halmashauri husika.<br><br>4.3.4 Kikosi Kazi kinapendekeza Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maliasili na Utalii wahakikishe kuwa mifugo yote iliyopo katika maeneo ya Hifadhi za Taifa, Hifadhi za Akiba na maeneo mengine yaliyoanishwa kwa shughuli zisizo za ufugaji inaondolewa haraka.<br><br>4.3.5 Kutokana na ongezeko kubwa la watu katika bonde, kuwepo na hatua za kudhibiti ongezeko la watu kwa kutoa elimu ya idadi ya watu kuwiana na matumizi endelevu ya raslimali za asili.<br><br>4.3.6 Jitihada zielekezwe katika kuongeza uzalishaji (productivity) badala ya kuongeza maeneo yanayolimwa. |
| 5.0 Kuanzisha na kuimarisha Taasisi | **5.1 Mapendekezo ya Kisera na Kisheria** |

| | |
|---|---|
| na Mifuko inayosimamia Maendeleo ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu | 5.1.1 Serikali iunde **Mamlaka Maalum** kisheria itakayokuwa na majukumu ya kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali zilizopo katika Bonde la Mto Ruaha. Pamoja na mamlaka hiyo uundwe **Mfuko Maalum** wa Wakfu (Trust Fund) ambao utachangiwa na wote wanaonufaika na rasilimali za Bonde na wadau wengine na usimamiwe kwa pamoja wadau hao (Serikali, sekta binafsi na wabia wa Bonde la Mto Rufiji) Taasisi hiyo iwe chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais.<br><br>Aidha, ili kutekeleza pendekezo hilo mpango uhusishe hatua mbili kuu (i) kwa kuanzia Mamlaka hiyo ianzishwe kwa kutumia **Sheria ya Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 kwa maana ya Eneo Lindwa (Enviromentally Protected Area) (**ii) na Baadaye itolewe Sheria Maalum ya Kuunda Mamlaka, Mfuko na utaratibu wa kuuchangia na kuusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za Bonde.<br><br>Kikosi Kazi kinatambua zipo mamlaka mbalimbali ambazo zimeundwa katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu/Rufiji hivyo, ufanyike mpango wa **kurazinisha** mipaka na majukumu ya mamlaka hizo ili ziweze kutekeleza majukumu yake chini ya Mamlaka Maalum na Mfuko. |
| | **5.2 Mapendekezo ya Kimkakati**<br><br>5.2.1 Mamlaka inayopendekezwa ihakikishe mipango na shughuli za sekta mbalimbali ndani ya Bonde inaratibiwe ili kuhakikisha inatekelezwa kwa utaratibu endelevu na inachangia katika maslahi mapana ya maendeleo ya Bonde badala ya kila taasisi na mipango yake.<br><br>5.2.2 Ili kuhakikisha usimamizi wa sera na sheria katika utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii katika Bonde, Mamlaka inayopendekezwa ipewe uwezo wa kuhakikisha kazi zote zinazotekelezwa katika Bonde zinazingatia sera na sheria zilizopo za uhifadhi wa mazingira na ikolojia ya Bonde.<br><br>5.2.3 Ili kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali maji katika eneo la Bonde yanakidhi mahitaji ya wadau wote, Mamlaka inayopendekezwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, ihakikishe kilimo cha umwagiliaji kinafanyika kulingana na sheria na taratibu zilizopo. Aidha, ifanyike tathmini ya kiasi cha maji katika kila chanzo, mahitaji katika skimu za umwagiliaji zilizopo kwa sasa na kulinganishwa na vibali vilivyotolewa. Teknolojia za kisasa |

| | |
|---|---|
| | zitumike katika kuongeza ufanisi katika miradi ya umwagiliaji. |
| 6.0 Kupitia na Kuboresha utekelezaji wa Sera na Sheria zinazohusu Usimamizi wa Bonde la Mto la Mto Ruaha Mkuu | 6.1 **Mapendekezo ya Kisera na Kisheria**<br>6.1.1 Ofisi ya Makamu wa Rais, ihakikishe Wizara za kisekta zinasimamia Sera na Sheria katika utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii katika Bonde. Mamlaka inayopendekezwa ipewe uwezo wa kuhakikisha kazi zote zinazotekelezwa katika Bonde zinazingatia Sera na Sheria zilizopo za uhifadhi wa mazingira na ikolojia ya Bonde.<br><br>6.1.2 Wizara za kisekta zikishirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria zifanye mapitio ya sera na sheria za sekta zinazohusika moja kwa moja katika utunzaji wa mazingira ya Bonde na nchini kwa ujumla ili kuhakikisha zina uwezo wa kuwezesha wadau kusimamia kwa ufanisi zaidi matumizi endelevu ya raslimali za Bonde na mazingira kwa ujumla. |

### *3.1.1 Usimamizi wa Matumizi Endelevu ya Rasilimali Maji*

**Lengo**

Kuboresha upatikanaji, usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za maji ndani ya bonde la Mto Ruaha Mkuu.

Umuhimu

Usimamizi na uratibu duni wa shughuli za kiuchumi na kijamii katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu umesababisha uharibifu mkubwa wa mazingira. Uharibifu huo umejidhihirisha katika maeneo mbalimbali ikiwemo upungufu mkubwa wa maji na mara nyingine kukauka kwa mito mbalimbali inayochangia maji kwenye Mto Ruaha Mkuu, ikiwemo kukauka kwa muda mrefu kwa Mto Ruaha Mkuu.

Historia inaonesha kwamba kabla ya miaka ya 1980, mtiririko wa maji katika Mto Ruaha Mkuu wakati wa kiangazi ulikuwa kati ya mita za ujazo 0.5 – 1.0 kwa sekunde. Kuanzia miaka ya 1990, mitiririko wa maji wakati wa kiangazi umepungua na kufikia mita za ujazo sifuri (0) wakati wa kiangazi. Uharibifu wa mazingira na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu, hasa kilimo cha umwagiliaji kisicho endelevu, ufugaji, upandaji wa miti ya kibiashara na uvunaji wa misitu usio endelevu na shughuli zingine za kibinadamu zimesababisha mtiririko wa maji katika mito na vijito kupungua na kukauka kwa muda mrefu kuliko ilivyokuwa hapo awali. Maeneo ya umwagiliaji hususan katika eneo la Usangu yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka kutoka hekta 14,000 mwaka 1980 mpaka hekta 24,000 mwaka 1990 na kufikia hekta za mraba 115,000 mwaka 2015 na kuchangia kupungua kwa mtiririko wa maji katika Mto Ruaha Mkuu mwaka hadi mwaka

**Mikakati**

Mikakati iliyowekwa ili kuimarisha usimamizi wa matumizi endelevu ya rasilimali maji ni pamoja na:

- Uanzishaji na kuimarisha jumuiya za watumia maji zilizopo;
- Kuimarisha usimamizi wa sheria zinazo simamia rasilimaji za maji;
- Kuongeza ujazo wa maji kwa kurejesha mito kwenye mikondo yake;
- Kuimarisha utunzaji wa vyanzo vya maji;
- Kuwa na taratibu endelevu za upatikanaji wa maji kwa kilimo cha umwagiliaji;
- Kuboresha ufanisi wa matumizi ya maji katika kilimo cha umwagiliaji; na
- Kuimarisha usimamiaji wa matumizi bora ya maji katika skimu zote za umwagiliaji.

**Shabaha**

1. Jumuiya 50 za watumia maji zimeanzishwa ifikapo Juni, 2018.
2. Mifumo na sheria za Jumuiya za watumia maji 29 zimeimarishwa ifikapo Juni, 2019.
3. Jumuia 29 za watumia maji zimejengewa uwezo ifikapo Juni, 2018.
4. Taasisi 7 zinazosimamia matumizi ya sheria za maji zimefanyiwa mafunzo ya usimamizi wa rasilimali maji ifikapo Desemba 2017.

5. Sheria 8 zinazohusu uhifadhi wa Rasilimali maji zinasimamiwa na kutekelezwa ipasavyo ifikapo Desemba 2017.
6. Mikondo 4 ya mito iliyopoteza uelekeo imerejeshwa ifikapo Juni, 2022.
7. Vyanzo vya maji vyote vimetambuliwa na kuhifadhiwa ifikapo Juni, 2020.
8. Skimu zote za umwagiliaji zimefanyiwa tathmini na zimezingatia sheria za maji na umwagiliaji ifikapo Desemba 2018.
9. Mabwawa matatu ya Lwanyo, Salimuwani na Lugoda Lutali yamejengwa ifikapo 2019.
10. Tathimini ya maji imefanyika kwenye mito na vibali vimehakikiwa ifikapo 2019.
11. Miundombinu ya umwagiliaji ya skimu 80 imeboreshwa ifikapo 2022.
12. Vyama vya wamwagiliaji maji vimeanzishwa na kuimarishwa kusimamia vyema rasilimali maji ifikapo 2019.
13. Teknologia zinazotumia maji kidogo kuzalisha mpunga zihameimarishwa na kutumika ifikapo 2019.

**Viashiria**

1. Asilimia ya Jumuiya za watumia maji zilizoanzishwa.
2. Asilimia ya Jumuiya za watumia maji zilizoimarisha Mifumo, mafunzo na sharia.
3. Asilimia ya Jumuiya za watumia maji zilizopata mafunzo kuhusiana na sharia.
4. Asilimia ya taasisi zilizopata mafunzo ya usimamizi wa rasilimali maji.
5. Idadi ya Sheria zinazosimamia matumizi ya rasilimali za maji zilizofanyiwa marekebisho.
6. Idadi ya sheria zinazohusu uhifadhi wa Rasilimali maji zinasimamiwa na kutekelezwa.
7. Asilimia ya mikondo ya mito iliyorejeshwa.
8. Asilimia ya vyanzo vya maji vilivyotambuliwa na kuhifadhiwa.
9. Orodha ya skimu zilizohakikiwa kufanyiwa tathmini.
10. Asilimia ya mabwawa yaliyojengwa na yanatumika.
11. Idadi ya Mito inayotiririsha maji baada ya kuondolewa mchanga.
12. Kiasi cha maji kilichopo.
13. Idadi ya vibali vilivyohakikiwa.
14. Asilimia ya vibali vilivyorekebishwa.
15. Asilimia ya mito imefanyiwa tathimini ya kiwango cha maji.
16. Asilimia ya skimu zilizoboreshwa miundombinu ya umwagiliaji.
17. Asilimia ya skimu zenye vipimo vya maji kwenye mifereji mikuu na mirefeji ya matoleo.
18. Orodha ya skimu zilizo na vyama vya wamwagiliaji.
19. Asilimia ya eneo lililo chini ya tekinologia zitumiazo maji kidogo kuzalisha mpunga.

### *3.1.2 Kuimarisha upatikanaji, Matumizi na Usimamizi endelevu wa Rasilimali Ardhi*

**Lengo**

Kuondoa migogoro ya matumizi ya ardhi na kulinda mazingira ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu

**Uhalali**

Bonde la Mto Ruaha Mkuu linabeba Wilaya 18 za vijijini na maeneo matano ya mjini ndani ya mikoa 7 ya kiutawala (Iringa, Njombe, Mbeya, Dodoma, Singida na Morogoro). Hali ilivyo kwa sasa inaonyesha kuwa Wilaya na Vijiji vingi havina mipango ya matumizi ya ardhi, aidha vijiji vichache vyenye matumizi ya ardhi havijahuisha mipango hiyo kuendana na mahitaji yaliyopo. Hali hii imesababisha kuwepo kwa matumizi makubwa ya ardhi yasioendana na hali halisi ya ukubwa wa Bonde, kukosekana kwa vipaumbele vya matumizi ya ardhi katika maeneo nyeti na kupelekea migogoro na uharibifu mkubwa wa mazingira.

Zinahitajika juhudi zitakazowezesha kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali ardhi ikiwemo kuandaa, kuhuisha na kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi inayotekelezeka; na kuweka ukomo wa kiwango cha juu cha ardhi ambacho inaweza kumilikiwa na kutumiwa kwa kilimo, Hifadhi za wanyamapori, misitu, vyanzo vya maji na ardhioevu, uendelezaji wa makazi, huduma za jamii, ufugaji, viwanda na matumizi mengine kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999 pamoja na kutekeleza Tangazo la Serilali Na. 28/2008.

**Mikakati**

- Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mipango ya matumizi ya Ardhi.
- Kuharakisha utekelezaji wa marekebisho ya Tangazo la Serikali Namba 28/ 2008.

**Shabaha**

1. Mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji vyote vilivyopo katika bonde la Mto Ruaha Mkuu imeandaliwa na kutekelezwa ifikapo 2019.
2. Uhakiki wa milki (hati) zote zilizotolewa katika ardhi oevu na vyanzo vya maji zimebatilishwa ifikapo 2019.
3. Tangazo la Serikali Namba 28/2008 limerekebishwa na limetekelezwa ifikapo 2018.
4. Maeneo yenye mwinamo mkali yasiyofaa kwa kilimo na makazi yamebainishwa na kuwekwa kwenye mpango wa ardhi ifikapo 2022.
5. Mipango iliyopo imepitiwa na imehuishwa ifikapo 2019.

**Viashiria**

1. Idadi ya vijiji vilivyofanyiwa mpango wa matumizi ya ardhi.
2. Idadi ya hati za hakimiliki zilizobatilishwa.
3. Tangazo jipya la Serikali la kurekebisha Tangazo Namba 28/2008.
4. Idadi ya maeneo yenye mwinuko mkali yasiyofaa kwa kilimo na makazi.
5. Asilimia ya maeneo yasiyofaa kwa kilimo na makazi yaliyowekwa kwenye mpango wa ardhi.
6. Asilimia ya mipango iliyopitiwa na kuhuishwa.

### *3.1.3 Kuimarisha Usimamizi endelelevu wa Mazingira, Hifadhi za Taifa na Misitu*

**Lengo**

Kuboresha uhifadhi wa mazingira ya Hifadhi za Taifa na misitu katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu.

**Uhalali**

Bonde la Mto Ruaha Mkuu lina utajiri wa mazingira mazuri yenye umuhimu na umaarufu mkubwa kitaifa na kimataifa zikiwemo Hifadhi nne za wanyamapori (Kitulo, Ruaha, Udzungwa na Mikumi), Mapori sita ya Akiba (Selous, Lunda, Kipengere-Mpanga, Rungwa, Kizigo na Muhesi), eneo la Ramsar la Rufiji - Mafia- Kilwa – (RUMAKI) na eneo lindwa la Ihefu.

Tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa wastani wa ukubwa wa ardhi oevu ya Ihefu, umepungua kutoka kilometa za mraba 180 kabla ya mwaka 1990 hadi 120 mwaka 2015. Eneo la Ng'iriama ambalo lilipitisha maji mwaka mzima kutoka Ihefu, sasa hivi hukosa maji kwa vipindi virefu vya mwaka. Mtiririko wa maji katika Mto Ruaha Mkuu ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha umekuwa ukikauka kwa miezi kati ya 4 – 6 kila mwaka kuanzia mwa miaka ya 1990. Ardhi oevu ya Ihefu, Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na uzalishaji umeme katika vituo vya mtera na kidatu vinaathiriwa kutokana na kukosekana kwa usimamizi endelevu wa rasilimali hizi.

**Mikakati**

- Kusimamia Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira, Tathmini ya Athari na Ukaguzi kwa Mazingira.
- Kuhakikisha Sekta zote zinazosimamia utekelezaji wa shughuli za kiuchumi katika Bonde zinajumuisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika Mipango, Mikakati na program.
- Uhifadhi wa uoto wa asili katika bonde.
- Kuanzisha mfumo wa malipo sawia kwa Huduma za Mazingira.

**Shabaha**

1. Tathmini ya Mazingira Kimkakati katika Sera, Sheria, Mikakati, na Programu imefanyika ifikapo 2018.
2. Ukaguzi wa mazingira kwa miradi inayotekelezwa na Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa miradi itakayotekelezwa ndani ya Bonde umefanyika ifikapo 2022.
3. Mipango, Mikakati na programu ya Sekta inayotekelezwa katika bonde inajumuiya masuala ya mabadiliko ya tabianchi ifikapo 2019.
4. Maeneo yenye uoto wa asili yametambuliwa na kuhifadhiwa ifikapo 2019.
5. Mfumo wa malipo sawia kwa Huduma za mazingira imeanzishwa na kutekelezwa ifikapo 2019.

**Viashiria**

1. Taarifa ya Tathmini ya Mazingira Kimkakati.
2. Idadi ya miradi iliyofanyiwa Tathmini ya Tthari kwa Mazingira.
3. Idadi ya miradi iliyofanyiwa Ukaguzi wa Mazingira.
4. Idadi ya Mipango, Mikakati na Programu iliyojumuisha masuala ya mabadiliko ya nchi.
5. Asilimia ya maeneo uoto wa asili yaliyohifadhiwa.

6. Idadi ya wadau wanaolipia Huduma za Mazingira.

### *3.1.4 Kusimamia shughuli endelevu za uzalishaji katika sekta za Nishati, Kilimo, Ufugaji, Uvuvi na Shughuli za Kijamii*

**Lengo**

Kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji endelevu wa Nishati ya umeme utokanao na maji katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu.

**Uhalali**

Bonde la Mto Ruaha Mkuu lina vituo vikuu viwili vinavyozalisha umeme kwa njia ya maji (Mtera na Kidatu) ambavyo hutegemewa kwa asilimia 41 ya uzalishaji wa umeme wa maji nchini Tanzania. Kwa wakati huu, vituo hivi vinazalisha chini ya asilimia 40. Tafiti zilizopo zinaonyesha kuwa uwezo wa bonde katika kuzalisha umeme wa maji ni mkubwa na tayari maeneo mbalimbali yameshatambuliwa ikiwa ni pamoja na maporomoko ya Stiegler's na kuingizwa kwenye Mpango Mkuu wa Sekta ya Umeme.Changomoto kubwa zitakazoathiri uwezo huo ni uharibifu wa mazingira unaoendelelea katika Bonde hili.

**Mikakati**

Kufanya tathmini ya ardhi oevu na vyanzo vya maji yanayochimbwa madini.

**Shabaha**

Maeneo oevu na vyanzo vya maji yanayochimbwa madini yamebainishwa ifikapo 2019.

**Viashiria**

Idadi ya maeneo oevu na vyanzo vya maji.

**Lengo**

Kuboresha matumizi ya maji katika shughuli za kilimo.

**Uhalali**

Hali ilivo kwasasa inaonyesha kuwa shughuli za kilimo zinachukua mpaka asilimia 84 ya matumizi yote ya maji kwa takwimu za mwaka 2010. Mahitaji haya yanatarajiwa kuongezeka mara 1.4 ifikapo 2035. Juhudi za maksudi zinahitajika ili kuhakikisha uzalishaji wa mazao ya kilimo unazingatia kilimo hifadhi katika maeneo yanayotegemea mvua na kilimo shadidi katika maeneo ya umwagiliaji.

**Mikakati**

Kusimamia kilimo hifadhi na kilimo shadidi.

**Shabaha**

Kilimo hifadhi na kilimo shadidi kinasimamiwa na kutekelezwa ifikapo 2019.

**Viashiria**

Asilimia ya wakulima wanaotekeleza kilimo hifadhi na kilimo shadidi.

**Lengo**
Kuhakikisha kuwa shughuli za ufugaji na uvuvi zinasimamiwa ipasavyo ili zilete tija na kutunza mazingira.

**Uhalali**

Kumekuwepo na ongezeko kubwa la mifugo lisiloendana na uwezo wa ardhi ya malisho iliyopo. Ukosefu wa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho na mabirika ya kunyweshea maji kumesababisha uchungaji holela kiasi cha mifugo kuvamia maeneo ya Hifadhi za Taifa, kuharibu kingo za mto na maeneo ya ardhi aoevu. Ni vema kuwa na idadi sahihi ya mifugo na maeneo ya malisho na mabirika ya kunyweshea mifugo ili kuepusha migogoro na kuokoa mazingira. Aidha, shughuli za uvuvi ambazo hazifuati sheria zinaharibu mazingira ya mito, ardhi oevu, mazalia ya samaki na mtiririko wa maji mtoni. Ni vema kuanzisha na kuhamasisha a ufugaji wa samaki ili kuokoa mazingira ya mito, ardhi oevu na mazalia ya samaki. Shughuli za kijamii kama uendelezaji wa makazi na huduma muhimu kama shule, zahanati, masoko na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na bararbara hufanyika pasipo mpango maalumu unazingatia matumizi endelevu ya ardhi na rasmali maji. Ni vema kuwa na mpango wa usimamizi endelelevu wa shughuli za huduma za jamii katika Bonde la Mto ruaha Mkuu.

**Mikakati**

- Uzalishaji wa mazao ya mifugo na uvuvi unafanyika kwa kutumia mbinu bora za uzalishaji.
- Kukamilisha utambuzi na uwekaji alama mifugo.
- Ujenzi wa miundombinu ya mifugo.
- Kuzuia shughuli za ufugaji kwenye maeneo oevu.

**Viashiria**

1. Mbinu bora za uzalishaji wa mazao ya mifugo ifikapo Juni, 2022.
2. Ukomo wa idadi ya mifugo katika Mto Ruaha Mkuu unawekwa ifikapo Juni, 2018.
3. Shughuli za kibinadamu kwenye maeneo oevu zimezuiliwa ifikapo Juni, 2017.
4. Miundombinu ya mifugo katika bonde imejengwa ifikapo Juni, 2022.
5. Uvuvi na ufugaji wa samaki endelevu kwenye mito, mabwawa na maeneo oevu umesimamiwa ifikapo Juni, 2020.

**Viashiria**

1. Asilimia ya wakulima, wafugaji na wavuvi wanaotumia mbinu bora za uzalishaji.
2. Asilimia ya mifugo iliyotambuliwa kwa kuwekwa alama.
3. Idadi ya mifugo inayoingia kutoka maeneo mengine katika bonde.
4. Tamko la kuzuia shughuli za ufugaji kwenye maeneo oevu.
5. Asilimia ya miundombinu ya mifugo iliyojengwa.

### *3.1.5 Kuanzisha na KuimarishaTaasisi na Mifuko inayosimamia maendeleo ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu*

**Lengo**

Kuwa na usimamizi endelevu wa rasilimali zilizopo katika bonde la Mto Ruaha Mkuu.

**Uhalali**

Mojawapo ya sababu zinazosababisha uharibifu wa mazingira katika bonde la Ruaha Mkuu ni pamoja na matumizi holela ya rasilimali, kukosekana kwa usimamizi na utekelezaji wa pamoja wa mipango na shughuli za kiuchumi na uwezo mdogo wa kifedha kwa taasisi zilizopo. Hivyo, kuundwa kwa taasisi na mfuko maalum wa Wakfu utakaosimamia shughuli zote za kiuchumi na kijamii katika bonde hili utasaidia matumizi endelevu ya rasilimali.

**Mikakati**

- Uanzishwaji wa Mamlaka maalum ya kusimamia na kuratibu matumizi endelevu ya rasilimali zilizopo katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu.
- Uanzishwaji wa Mfuko maalum wa Wakfu wa Mamlaka.

**Shabaha**

1. Maeneo tekechu (environmental sensitive areas) ndani ya bonde yametangazwa kuwa maeneo lindwa ifikapo 2021.
2. Mamlaka maalum ya kusimamia na kuratibu matumizi endelevu ya rasilimali zilizopo katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu imeanzishwa ifikapo 2022.
3. Mfuko Maalum wa Wakfu wa Mamlaka umeanzishwa ifikapo 2022.
4. Majukumu mbalimbali ya Taasisi zilizopo ndani ya bonde yameainishwa ifikapo 2020.

**Viashiria**

1. Uwepo wa maeneo lindwa.
2. Uwepo wa Mamlaka maalum.
3. Uwepo Mfuko maalum wa Wakfu chini ya Mamlaka.
4. Uwepo wa usimamizi wa pamoja.
5. Uwepo wa majukumu ya kila taasisi.

### *3.1.6 Kupitia na Kuboresha utekelezaji wa Sera na Sheria zinazohusu Usimamizi wa Bonde la Mto Ruaha Mkuu*

**Lengo**

Kuwa na utekelezaji bora wa Sera na Sheria zinazosimamia Bonde la Mto Ruaha Mkuu ili kuimarisha matumizi ya rasilimali zilizopo. Elimu kuhusu Sheria na Sera hizo zinatolewa kwa wasimamizi, watekelezaji na wananchi.

**Uhalali**

Tanzania tuna Sera na Sheria mbalimbali za kisekta zinazosimamia matumizi ya rasilimali za asili katika mabonde ya mito mikuu ikiwemo bonde la Mto Ruaha Mkuu lakini utekelezaji wake umekumbana na changamoto za mara kwa mara. Kwa sehemu changamoto hizo zinasababishwa na kukosekana kwa uratibu wa usimamizi na utekelezaji wa Shera na Sera za kisekta pia kuna udhaifu wa elimu kuhusu sheria hizo kwa wasimamizi na watekelezaji. Kutokana na kuongezeka kwa athari za kimazingira zitokanazo na matumizi yasiyo endelevu, serikali imeazimia kupitia na kuboresha utekelezaji wa Sera na Sheria zinazohusu Usimamizi wa Bonde la Mto Ruaha.

**Mkakati**

Kuboresha utekelezaji wa Sera na Sheria zinazohusu Usimamizi wa Bonde la mto Ruaha Mkuu.

**Shabaha**

Sera na Sheria zinazohuzu usimamizi wa Bonde la Mto Ruaha Mkuu zinatekelezwa kwa ukamilifu ifikapo June, 2018.

**Kiashiria**

Uzingatiaji wa Sera na Sheria katika matumizi ya rasilimali za Bonde la Mto Ruaha Mkuu.

***3.1.7 Kuboresha uratibu wa shughuli za usimamizi wa Bonde la Mto Ruaha Mkuu.***

**Lengo**

Uratibu wa shughuli za usimamizi wa Bonde la Mto Ruaha Mkuu unakuwa imara na wenye ufanisi ili kushughulikia masuala ya kimaendeleo katika bonde hilo.

**Uhalali**

Mamlaka mbalimbali kama RUBADA na Wizara za Sekta ya Kilimo na Maliasili zinatekeleza shughuli za uchumi na uhifadhi mazingira katika bonde la Mto Ruaha Mkuu lakini bado usimamizi wa matumizi ya rasilimali unakumbana na changamoto nyingi zinazochangiwa na uratibu hafifu. Hakuna usimamizi wa pamoja wa Mipango, Sera na Sheria za usimamizi wa maendeleo ya uchumi pamoja na mazingira katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu. Ili kuboresha uratibu wa shughuli za uhifadhi wa bonde kuna haja ya kuanzisha chombo cha usimamizi cha mpito (kamati wezeshi) kwa kushirikisha sekta binafsi na serikali kuu. Kamati wezeshi itafanya kazi mpaka pale Mamlaka pendekezwa itakapoanzishwa.

**Mikakati**

- Uanzishwaji wa Kamati Wezeshi ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu.
- Uratibu wa pamoja wa shughuli za Usimamizi wa Bonde la Mto Ruaha Mkuu.
- Kufanya tafiti mbalimbali kuhusu ikolojia ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu.

**Shabaha**

1. Kamati wezeshi ya usimamizi wa pamoja wa Bonde la Mto Ruaha Mkuu imeanzishwa ifikapo Juni, 2017.
2. Uratibu wa pamoja wa usimamizi Rasilimali za Bonde la Mto Ruaha Mkuu unakuwepo ifikapo Juni, 2017.
3. Tafiti mbalimbali za kutatua changamoto za hifadhi ya mazingira katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu zinafanyika ifikapo Juni 2020.

**Viashiria**

1. Uwepo wa Kamati wezeshi.
2. Mpango wa uratibu wa pamoja.
3. Idadi ya Mikutano ya Uratibu.
4. Idadi ya Mipango, Mikakati, Programu na Miradi iliyoratibiwa kwa pamoja.
5. Idadi ya tafiti zilizofanyika.

*Majedwali ya Mpango Kazi: Rasimu ya Mpango kazi wa Kitaifa wa Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu*

### 3.1.1 Eneo: Usimamizi wa matumizi endelevu ya Rasilimali maji

**Lengo: Kuboresha upatikanaji, usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za maji ndani ya bonde la Mto |Ruaha Mkuu**

| Matokeo/Shabaha | Shughuli | Muda wa utekelezaji | Viashiria | Wahusika | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mhusika Mkuu | Wahusika Wengineo |
| **3.1.1.1** Jumuiya 50 za watumia maji zimeanzishwa ifikapo Desemba, 2018 | **3.1.1.1.1** Kubainisha vyanzo vya maji ambavyo havina Jumuiya za Watumia maji | Juni, 2017 - Disemba 2018 | Idadi ya vyanzo vya maji vilivyobainishwa | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji; NEMC; NIRC; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD;LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.1.2** Kuziwezesha timu za Wataalamu wa Maji na Usafi wa Mazingira ya Wilaya kufanya mikutano 50 ili kuanzisha mchakato wa kuunda Jumuiya za watumia maji | Juni,2017-Juni,2018 | Idadi mikutano ya mchakato wa kuanzisha Jumuiya za watumia maji | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji; NEMC; NIRC; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD;LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.1.3** Kuandaa rasimu za Katiba na kanuni ya Watumia maji | Juni,2017 hadi Disemba 2018 | Rasimu za Katiba na Kanuni | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji; NEMC; NIRC; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD ;LGAs; |

| Matokeo/Shabaha | Shughuli | Muda wa utekelezaji | Viashiria | Wahusika | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mhusika Mkuu | Wahusika Wengineo |
| | | | | | SAGCOT |
| | **3.1.1.1.4** Kusajili Jumuiya 21 za watumia maji | Juni, 2017 - Disemba 2018 | Asilimia ya Jumuiya za Watumia maji zimeanzishwa | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br>NEMC; NIRC; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD;<br>LGAs; SAGCOT |
| **3.1.1.2** Kujenga uwezo kwa Jumuiya za watumia maji 29 kuifika Juni, 2019 | **3.1.1.2.1** Kutoa elimu kwa Jumuiya za watumiaji maji kuhusu sheria za usimamizi wa rasilimali maji | Juni, 2017 –Juni, 2019 | Asilimia ya Watumiaji maji wanaopata elimu usimamizi wa rasilimali maji | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br>NEMC; NIRC; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD;<br>LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.2.2** Kuziwezesha Jumuiya za watumia maji kubainisha na kuweka mipaka kwenye vyanzo vya maji | Juni, 2017 –Juni, 2019 | Asilimia ya Vyanzo vya maji vilivyobainishwa na kuwekewa mipaka | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br>NEMC; NIRC; RS; TAMISEMI; OMR; |

| Matokeo/Shabaha | Shughuli | Muda wa utekeleza ji | Viashiria | Wahusika | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mhusika Mkuu | Wahusika Wengineo |
| | | | | | MLHHSD;<br>LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.2.3** Kuandaa Mikataba ya Makubaliano ya kuziwezesha Jumuiya za watumia maji kunufaika na jitihada za uhifadhi kama sehemu ya motisha | Juni, 2017 –Juni, 2019 | Namba ya Mikataba iliyofikiwa makubalinao | Wizara ya Maji na Umwagiliaj i | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br>NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD;<br>LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.2.4** Kuandaa ziara 10 za mafunzo kuhusu mifumo ya usimamizi wa Rasilimaji za maji kwa Jumuiya za Watumia maji | Juni, 2017 –Juni, 2019 | Idadi ya ziara za mafunzo | Wizara ya Maji na Umwagiliaj i | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br>NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD;<br>LGAs; SAGCOT |
| **3.1.1.3** Jumuia 29 za watumia maji zimejengewa uwezo ifikapo Juni, 2018 | **3.1.1.3.1** Kuandaa Mwongozo wa kutoa elimu kwa Jumuiya za watumiaji maji kuhusu sheria za usimamizi wa rasilimali | Juni, 2017 – Juni, | Uwepo wa Mwongozo wa kutoa elimu kwa | Wizara ya Maji na Umwagiliaj | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji; |

| Matokeo/Shabaha | Shughuli | Muda wa utekelezaji | Viashiria | Wahusika | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mhusika Mkuu | Wahusika Wengineo |
| | maji | 2018 | Jumuiya za watumiaji maji kuhusu sheria za usimamizi wa rasilimali maji | i | NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD; LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.3.2** Kuendesha Warsha 3 za kutoa elimu kwa Jumuiya za watumiaji maji kuhusu sheria za usimamizi wa Rasilimali maji | Juni, 2017 – Juni, 2018 | Asilimia ya Jumuiya za watumia maji zimepata elimu kuhusu sheria za usimamizi wa Rasilimali maji | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji; NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD; LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.3.3** Kuandaa vipeperushi 1,000 vyenye lugha nyepesi kuhusiana na sheria ya uhifadhi rasilimali maji na mazingira | Juni, 2017 – Juni, 2018 | Idadi ya vipeperushi vilivyoandaliwa | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji; NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD; LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.3.4** Kuandaa Makala 10 kwenye Radio/TV programu | Juni, 2017 – Juni, | Idadi ya makala zilizoandaliwa | Wizara ya Maji na | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji; |

| **Matokeo/Shabaha** | **Shughuli** | **Muda wa utekelezaji** | **Viashiria** | **Wahusika** | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mhusika Mkuu | Wahusika Wengineo |
| | | 2018 | | Umwagiliaji | NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD;<br>LGAs; SAGCOT |
| **3.1.1.4** Taasisi 7 zinazosimamia matumizi ya sheria za maji zimefanyiwa mafunzo ya usimamizi wa rasilimali maji ifikapo Desemba 2017 | **3.1.1.4.1** Kuandaa Miongozo ya kutoa elimu ya usimamizi wa rasilimali maji kwa Taasisi zinazosimamia sheria za maji | Juni, 2017 – Juni, 2018 | Uwepo wa Miongozo | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br>NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD;<br>LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.4.2** Kuandaa Warsha 3 za kutoa elimu ya usimamizi wa rasilimali maji kwa Taasisi zinazosimamia sheria za maji | Juni, 2017 – Juni, 2018 | Idadi ya warsha zimefanyika | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br>NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD;<br>LGAs; SAGCOT |
| **3.1.1.5** Sheria 8 zinazohusu uhifadhi wa Rasilimaji maji | **3.1.1.5.1** Kuandaa miongozo ya kutoa ufafanuzi kuhusiana na kifungu cha sheria cha mita | Juni - Desemba | Uwepo wa Miongozo | NEMC | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji; Wizara ya Maji na |

| Matokeo/Shabaha | Shughuli | Muda wa utekeleza ji | Viashiria | Wahusika | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mhusika Mkuu | Wahusika Wengineo |
| zinasimamiwa na kutekelezwa ipasavyo ifikapo Desemba 2017 | 60 | 2017 | | | Umwagiliaji NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD;<br>LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.5.2** Kutoa mafunzo ya tafsiri ya sheria 8 zinazohusu uhifadhi wa rasilimaji maji kwa watendaji katika Ngazi zote | Juni, 2017 – Juni, 2018 | Idadi ya Watendaji waliopata mafunzo | Wizara ya Maji na Umwagiliaj i | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br>NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD;<br>LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.5.3** Kufanya ufuatiliaji wa pamoja wa utekelezaji na uzingatiaji wa sheria 8 zinazohusu uhifadhi wa Rasilimaji maji katika wilaya 6 | Juni, 2017 – Juni, 2022 | Asilimia ya uzingatiaji wa sheria 8 wa watumiaji Rasilimali maji | Wizara ya Maji na Umwagiliaj i | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br>NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD;<br>LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.5.4** Kufanya uhakiki wa watu waliokiuka sheria na taratibu | Juni 2017 – Juni | Hatua | NEMC | Ofisi ya Makumu wa Rais; Bodi ya Bonde |

| Matokeo/Shabaha | Shughuli | Muda wa utekelezaji | Viashiria | Wahusika | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mhusika Mkuu | Wahusika Wengineo |
| | mbalimbali zinazohusiana rasilimali za bonde na kuwachukulia hatua | 2018 | zilizochukuliwa<br><br>Idadi ya watu, taasisi, kampuni waliochukuliwa hatua<br><br>Asilimia ya waliochukuliwa hatua | | la Mto Rufiji;<br><br>NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD; TANAPA<br><br>LGAs; SAGCOT |
| **3.1.1.6** Mito minne iliyopoteza mikondo yake imerejeshwa na kuwekewa vichuja mchanga ifikapo Juni 2022 | **3.1.1.6.1** Kuhakiki maeneo ya mito yaliyopoteza mikondo na maeneo ya kujenga vichuja mchanga kwenye mito husika | Juni, 2017 – Juni, 2018 | Urefu wa maeneo ya mito iliyopoteza mikondo<br><br>Kutambuliwa kwa maeneo ya kujengewa vichuja mchanga | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br><br>NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD;<br><br>LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.6.2** Kufanya upimaji wa maeneo yaliyopoteza mikondo (Top survey) | Juni, 2017 – Juni, 2018 | Taarifa ya upimaji ya maeneo yaliyopeza | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br><br>NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; |

| Matokeo/Shabaha | Shughuli | Muda wa utekelezaji | Viashiria | Wahusika | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mhusika Mkuu | Wahusika Wengineo |
| | | | mikondo | | OMR; MLHHSD;<br>LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.6.3** Kufanya usanifu wa kina na kukokotoa gharama za kuondoa mchanga maeneo ya mito yaliyopoteza mikondo | Juni, 2017 – Juni, 2019 | Gharama za kuondoa mchanga maeneo ya mito yaliyopoteza mikondo | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br>NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD;<br>LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.6.4** Kuandaa makabrasha ya zabuni na kufanya taratibu za manunuzi ya wakandarasi na kusainiana mikataba | Juni, 2017 – Juni, 2019 | Idadi ya Wakandarasi | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br>NEMC; NIRC; AG; ~~RS;~~ OR-TAMISEMI; OMR; MLHHSD;<br>LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.6.5** Kupima, kusanifu na kupata gharama za ujenzi wa vichujio mchanga | Juni, 2017 – Juni, 2019 | Taarifa za upimaji, usanifu, gharama za ujenzi | Wizara ya Maji na Umwagiliaj | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br>NEMC; NIRC; AG; |

| **Matokeo/Shabaha** | **Shughuli** | **Muda wa utekelezaji** | **Viashiria** | **Wahusika** | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mhusika Mkuu | Wahusika Wengineo |
| | | | | i | RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD;<br>LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.6.6** Kuandaa makabrasha ya zabuni, kununua wakandarasi na kuanza kazi | Juni, 2018 – Juni, 2019 | Mikataba ya kuanza kazi | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br>NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD;<br>LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.6.7** Kufukua mchanga kwenye mikondo ya mito iliyopotea | Juni, 2018 – Juni, 2022 | Idadi mito iliyofukuliwa mikondo yake | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br>NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD;<br>LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.6.8** Kujenga vizuizi vya mchanga kwenye mikondo ya mito minne kwenye ukanda wa juu (Up streams) | Juni, 2017 – Juni, 2018 | Idadi ya vizuizi vya mchanga | Wizara ya Maji na Umwagiliaj | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br>NEMC; NIRC; AG; |

| Matokeo/Shabaha | Shughuli | Muda wa utekelezaji | Viashiria | Wahusika | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mhusika Mkuu | Wahusika Wengineo |
| | | | | i | RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD;<br>LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.6.9** Kufukia Mifereji yote isiyo rasmi katika mito 4 | Juni, 2017 – Juni, 2022 | Idadi ya Mifereji iliyofukiwa | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br>NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD;LGAs; SAGCOT |
| **3.1.1.7** Vyanzo vya maji vyote vimetambuliwa na kuhifadhiwa ifikapo Juni, 2022. | **3.1.1.7.1** Kuainisha vyanzo vikuu vya maji vyote katika Wilaya 6 zilizopo katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu | Desemba 2017. | Asilimia ya vyanzo vya maji vilivyobainishwa | OR TAMISEMI; | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br>NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD;<br>LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.7.2** Kupima rasmi mipaka kwenye vyanzo vya maji vyote vilivyobainishwa na kumilikishwa | Juni, 2017 – Juni 2022 | Idadi ya vyanzo vya maji vilivyopimwa na | MLHHSD | Wizara ya Maji na Umwagiliaji Bodi ya Bonde la Mto Rufiji; |

| Matokeo/Shabaha | Shughuli | Muda wa utekelezaji | Viashiria | Wahusika | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mhusika Mkuu | Wahusika Wengineo |
| | | | kumilikishwa | | NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR;<br>LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.7.3** Kubainisha na kuondoa miti isiyo rafiki kwenye vyanzo vyote vya maji. | Juni, 2017 – Juni 2020. | Idadi ya miti isiyo rafiki wa maji iliyobainishwa na kuondolewa katika vyanzo vya maji | MNRT | Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br>NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD<br>LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.7.4** Kupanda miti rafiki na maji kwenye vyanzo vya maji | Juni, 2017 – Juni 2022 | Idadi ya miti rafiki na maji iliyopandwa kwenye vyanzo vya maji | MNRT | Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br>NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD |

| **Matokeo/Shabaha** | **Shughuli** | **Muda wa utekeleza ji** | **Viashiria** | **Wahusika** | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mhusika Mkuu | Wahusika Wengineo |
| | | | | | LGAs; SAGCOT |
| | **3.1.1.7.5** Kuandaa miongozo ya aina na ukomo wa miti ya kupanda katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu | Juni, 2017 – Juni 2020 | Uwepo wa miongonzo | MNRT | Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Bodi ya Bonde la Mto Rufiji;<br><br>NEMC; NIRC; AG; RS; TAMISEMI; OMR; MLHHSD<br><br>LGAs; SAGCOT |
| **3.1.1.8** Skimu zote za umwagiliaji zimefanyiwa tathmini na zimezingatia sheria za maji na umwagiliaji ifikapo Desemba 2018 | **3.1.1.8.1** Kubainisha skimu za umwagiliaji zote na kuzifanyia tathimini | Juni, 2017– Juni, 2022 | Orodha ya skimu zilizohakikiwa | NIRC | Bonde la Mto Rufiji<br><br>RS; LGAs NEMC; TAMISEMI; |
| **3.1.1.9** Mabwawa matatu ya Lwanyo, Salimuwani na Lugoda Lutali | **3.1.1.9.1** Kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabwawa ya Lugoda lutali | Juni 2017 – Juni | Mabwawa yaliyofanyiwa | Wizara ya Maji na Umwagiliaj | Bonde la Mto Rufiji<br><br>RS; LGAs NEMC; |

| Matokeo/Shabaha | Shughuli | Muda wa utekelezaji | Viashiria | Wahusika | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mhusika Mkuu | Wahusika Wengineo |
| yamejengwa ili kuhifadhi maji na kusaidia mtiririko wa mto Ruaha ifikapo 2022 | na Salimuwani | 2019 | upembuzi yakifu | i | TAMISEMI |
| | **3.1.1.9.2** Kukamilisha ujenzi wa bwawa la Lwanyo | Juni 2017 – Juni 2019 | Bwawa la Lwanyo linatumika | Wizara ya Maji na Umwagiliaji i | RBWO<br>RS; LGAs; NEMC |
| | **3.1.1.9.3** Kufanya usanifu wa kina na kukokotoa gharama za ujenzi wa mabwawa | Juni 2017 – Juni 2019 | Taarifa ya usanifu wa kina na gharama za ujenzi wa mabwawa | Wizara ya Maji na Umwagiliaj i | Bonde la Mto Rufiji<br>RS; LGAs NEMC; TAMISEMI |
| | **3.1.1.9.4** Kufanya ujenzi wa mabwawa ya Lugodalutali na Salimuwani | Juni 2018 – Juni 2021 | Idadi ya Mabwawa yaliyokamilika | Wizara ya Maji na Umwagiliaj i | Bonde la Mto Rufiji<br>RS; LGAs NEMC; TAMISEMI |
| **3.1.1.10** Tathmini ya maji imefanyika kwenye mito na vibali | **3.1.1.10.1** Kufanya tathmini ya kiasi cha maji kwenye mito yote | Juni 2017 – Juni | Kiasi cha maji kilichopo | Wizara ya Maji na Umwagiliaj | Bonde la Mto Rufiji<br>RS; LGAs NEMC; |

| Matokeo/Shabaha | Shughuli | Muda wa utekeleza ji | Viashiria | Wahusika | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mhusika Mkuu | Wahusika Wengineo |
| vimehakikiwa ifikapo 2019 | | 2018 | | i | TAMISEMI |
| | **3.1.1.10.2** Kutoa vibali vya maji kulinagana na kiasi cha maji kilichopo | Juni 2017 – Juni 2019 | Idadi ya vibali vya maji vilivyotolewa | Wizara ya Maji na Umwagiliaj i | Bonde la Mto Rufiji<br><br>RS; LGAs NEMC; TAMISEMI |
| **3.1.1.11** Miundombinu ya umwagiliaji katika skimu zote katika bonde la Ruaha zimeboreshwa ifikapo 2022 | **3.1.1.11.1** Kubainisha skimu zote ambazo vyanzo vikuu vya upotevu wa maji ni kupitia miundombinu inayotumika | Juni,2017 – Juni,2022 | Idadi ya skimu zilizobainishwa | NIRC | Bonde la Mto Rufiji<br><br>RS; LGAs NEMC; TAMISEMI |
| | **3.1.1.11.2** Kufanya upembuzi yakinifu wa skimu zote zilizolengwa kuboreshwa | Juni, 2017– Juni, 2020 | Asilimia ya skimu zilizofanyiwa upembuzi yakinifu | NIRC | Bonde la Mto Rufiji<br><br>RS; LGAs NEMC; TAMISEMI |
| | **3.1.1.11.3** Kufanya usanifu wa kina na kukokotoa gharama za ujenzi kwa skimu zote | Juni, 2017– Juni, 2020 | Asilimia ya skimu zilizofanyiwa usanifu | NIRC | Bonde la Mto Rufiji<br><br>RS; LGAs NEMC; TAMISEMI |

| Matokeo/Shabaha | Shughuli | Muda wa utekelezaji | Viashiria | Wahusika | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mhusika Mkuu | Wahusika Wengineo |
| | **3.1.1.11.4** Kuandaa makaburasha ya zabuni na kufanya taratibu za manunuzi ya wakandarasi | Juni, 2018– Juni, 2022 | Idadi ya Wakandarasi | NIRC | Bonde la Mto Rufiji<br><br>RS; LGAs NEMC; TAMISEMI; |
| | **3.1.1.11.5** Kuweka vipimo vya maji kwenye mifereji inayoingiza maji na ya matoleo | Juni 2017 – June 2018 | Idadi ya mifereji iliyowekewa vipimo | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Bonde la Mto Rufiji<br><br>RS; LGAs NEMC; TAMISEMI |
| **3.1.1.12** Vyama vya wamwagiliaji maji vimeanzishwa na kuimarishwa kusimamia vyema rasilimali maji ifikapo 2019 | **3.1.1.12.1** Kuainisha skimu zote za umwagiliaji ambazo hazina vyama vya umwagiliaji | Juni 2017 – January 2018 | Idadi za skimu ya zisizikuwa na vyama vya wamwagiliaji | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji,<br><br>RS; LGAs; NEMC |
| | **3.1.1.12.2** Kuunda vyama vya wamwagiliaji | Juni 2017 – June 2019 | Asilimia ya skimu zilizo na vyama vya wamwagiliaji | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | Bodi ya Bonde la Mto Rufiji,<br><br>RS; LGAs; NEMC, TAMISEMI |
| | **3.1.1.12.3** Kuharakisha utekelezaji wa Mfuko wa Taifa wa Umwagiliaji. | June 2017 - 2018 | Mfuko wa Taifa wa Umwagiliaji unaofanya kazi | Wizara ya Maji na Umwagiliaji. | Wizara ya Fedha na Mipango, LGAs, RS, TAMISEMI, RWBO, SAGCOT. |

